JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Namba za simu
Mkuu wa shule 0769072265
Makamu Mkuu wa Shule 0688227012
Matroni/Patroni 0767908238

Shule ya sekondari MALAMPAKA
S.L.P 82, MALAMPAKA-SIMIYU
14/05/2018

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……
……..……
S.L.P ……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MALAMPAKA HALMASHAURI YA MASWA MKOA SIMIYU MWAKA 2018/2019.

1. Nafuahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya HGL/HGK/CBG. Shule ya Sekondari **MALAMPAKA** ipo umbali wa Kilometa 2 Mashariki mwa mji wa **MALAMPAKA.** usafiri wa basi kutoka mjini MZA/SHY/MSW unapatikana katika kituo cha mabasi **NYEGEZI/SHY/MSW** nauli ni shilingi 4000-8000, kutegemea unakotokea.

   Muhula wa masomo unaanza 02/07/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni 02/07/2018 Mwisho wa kuripoti ni 30/07/2018.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-
2.1.Sare ya shule

(a) Sare ya shule hii ni suruali 2 nyeusi rinda 2 na mfuko 1 nyuma, mashati meupe 2 mikono mirefu.

(b) Sare ya michezo ni Tracksouit 1 rangi ya bluu.

(c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi

(d) Soksi jozi mbili nyeusi za shule

(e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi

(f) Sweta rangi ya bluu yenye mikono ya kuishia begani.

(g) Nguo za kushindia (Shamba dress) suruali 1 kaki rinda 2 na mfuko 1 nyuma,

(h) Tai 2 zenye rangi ya suruali ya shule.

2.2.Ada na michango ya shuleni

A. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000 kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi shilingi 35,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 30801100097** katika Benki ya **NMB** (tafadhali andika **jina la mwanafunzi** kwenye pay in slip) **(MALAMPAKA SEC. SCHOOL REV.COLLECTION)**

B. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani .

(ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.

(iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.

(iv) Shilingu 30,000 kwa ajili ya kuwalipa wapishi,walinzi na vibarua wengine

(v) Shilingi 2,000/= nembo ya shule.

(vi) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tshs. 5,000/= na Bima ya Afya Tshs. 5,000/= (wanafunzi washauriwe kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya

(vii) Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima Mock.

(viii) Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa).

ANGALIZO: Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi ni shilingi 178,000/=

C. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

(i) Ream 1 ya karatasi (kwa mwaka).

(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa biolojia.

(iv) Scientific calculator CBG tu.

(v) Godoro kwa wanafunzi wa bweni.

(vi) Mashuka pair 2 , blanket 1, foronya 1 rangi ya bluu na chandarua 1

(vii) Vyombo vya chakula(sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

(viii) Ndoo mbili zenye mifuniko

(ix) Jembe 1 na Reki 1/ mfagio wa ndani 1 na nje 1.

2. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa sususi uliokubalika na uongozi wa shule.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa.

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovnja sheria za nchi.

(xiii) Kusababisha mimba zu kumpa mimba msichana

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba zakulala wageni

(xv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatanisho na Fomu muhimu

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Picha nne(4)za Wazazi na ndugu wa katibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA MALAMPAKA SEKONDARI.



GWEYA J. E.

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUPIMA AFYA

Mwanafunzi.....Andika ndiyo katika nafasi mbele ya ugonjwa ambao ulikwishaugua au unaugua:

(i) Kifua kikuu.....
(ii) Ugonjwa wa moyo.....
(iii) Ugojwa wa figo.....
(iv) Ugonjwa wa akili.....
(v) Ajali kubwa.....
(vi) Pumu.....
(vii) Vidonda vya tumbo.....
(viii) Kifafa.....
(ix) Kupasuliwa.....
(x) Ulemavu.....

KWA MATUMIZI YA KIOFISI TU MGANGA MKUU WILAYA/MKOA.

Tafadhali mpime mtajwa kama afya yake ina mruhusu aendelee na masomo ya Sekondari kidato cha TANO.

Pamoja na haya zingatia maelezo ya mwanafunzi hapo juu.

MAELEZO YA MGANGA.

.....
.....
.....

JINA LA MGANGA MKUU.....

SAINI NA MUHURI.....

CHEO.....

TAREHE.....

TAARIFA JUU YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

1. Jina kamili.....
2. Umri.....
3. Kazi.....
4. Anuani ya nyumbani, namba ya simu za Mzazi/Mlezi.....

   (i) Kijiji.....Wilaya.....

   (ii) Kata.....Mkoa.....

   (iii) Tarafa.....Uraia.....

5. Anuani kamali ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo .....

6. Anwani ya kazini ikiwa inatofautiana na hiyo apo juu kila inapobadilika utuarifu rasmi kwa barua.

7. Nathibitisha kwamba habari zitolewazo hapo juu ni kamili na kweli
   Jina la mzazi/mlezi.....
   Sahihi.....
   Tarahe.....

Ninaahidi wakati wote kushirikiana na kusaidiana na walimu katika kumlea kijana wangu awe na Tabia nzuri siku zote, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule.Juu ya hayo naelewa kuwa mwanangu akienda kinyume na kifungu cha sheria za shule, hatua za kinidhamu zitafuata ikiwemo kufukuzwa shule.

Jina la mzazi/mlezi.....

Saini.....

Tarehe.....